



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA



TAARIFA KWA UMMA

KUSITISHA MKATABA NA VITUO VYA MATIBABU VILIVYOKIUKA MASHARTI YA MKATABA

Dodoma, Jumatano, Juni 7, 2023:

1. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unapenda kuwatangazia Wanachama wake na Umma kuwa imesitisha mkataba wa kutoa huduma za matibabu kwa wanachama wake kwa vituo 11 kutokana na kukiuka mkataba na kuwasilisha madai ya malipo ya huduma yaliyobainika kuwa na udanganyifu.
2. Jukumu mojawapo la NHIF ni kulipa madai halali ya Watoa huduma za matibabu baada ya kuwahudumia wanachama wake kulingana na makubaliano. Katika kaguzi na chunguzi mbalimbali ambazo Mfuko unazifanya, umeendelea kubaini ukiukwaji wa makubaliano na vitendo vya udanganyifu vinavyofanywa na baadhi ya Watoa Huduma wasio waaminifu vyenye lengo la kujipatia mapato ya ziada yasiyo halali. Kutokana na hilo, Mfuko umeendelea kuchukua hatua stahiki kwa wanaobainika ikiwa ni pamoja na kusitisha mkataba na kuviwasilisha kwenye mamlaka za kisheria kwa hatua zaidi.
3. Vituo vifuatavyo vimesitishiwa mkataba:-

Na.	Jina la Kituo	Mkoa
1	Fface Polyclinic	Dar es Salaam
2	PCMC Polyclinic - Ilala	Dar es Salaam
3	Face Dental Specialized Clinic - Kinondoni	Dar es Salaam
4	Save Africa Polyclinic	Dar es Salaam
5	One Health Polyclinic	Dar es Salaam
6	DECCA Polyclinic	Dodoma
7	Hussain Specialized Polyclinic	Dar es Salaam
8	St Raphael Health Centre	Dar es Salaam
9	Nzega Polyclinic	Tabora
10	Mwaisela Health Centre	Tabora
11	Alphacare Polyclinic	Dodoma

4. Mfuko unawahakikishia wanachama wake kuwa huduma zinaendelea kupatikana katika vituo zaidi ya 9,000 nchi nzima vikiwemo vya Umma na Binafsi hivyo, unawataarifu kuendelea kutumia vituo vingine vyenye mkataba na NHIF vilivyo kwenye maeneo yao kupata huduma za matibabu kwa kutumia kadi zao za NHIF.
5. Mfuko unaendelea na kaguzi zake na kuchukua hatua stahiki kwa wanaobainika kufanya udanganyifu hivyo, unaendelea kuwahimiza Watoa huduma wenye mikataba na NHIF, wanachama na wadau kwa ujumla kuulinda Mfuko huu ili uweze kuwa endelevu katika kuwahudumia wananchi kwa kuwapa uhakiki wa matibabu na kuendelea kuwa chanzo kikubwa cha mapato kwa vituo.

Imetolewa na,

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA


Anjela Mziray
MENEJA UHUSIANO

Jengo la NHIF Tambukareli, Barabara ya Jakaya Kikwete, S. L.P 1437, Dodoma, Simu: +255 26 2 963 888,
Barua pepe: info@nhif.or.tz, Tovuti: www.nhif.or.tz